JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MTWARA 28/04/2020

OPARESHENI ZA UFUATILIAJI FEDHA ZA MALIPO YA KOROSHO, VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI NA SACCOS ZAZAA MATUNDA.
ZAIDI YA MILIONI 770 ZAREJESHWA.

Ndugu Waandishi wa Habari,

UTANGULIZI:

Nimewaita hapa kwa lengo la kuujulisha umma juu ya utendaji kazi wa TAKUKURU mkoa wa Mtwara kwa kipindi cha Januari – Machi 2020 Utaratibu huu ni wa kawaida ambao TAKUKURU imejiwekea ili kuhakikisha kuwa umma wa watanzania pamoja na wakazi wa mkoa wa Mtwara wanafahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2020 TAKUKURU (M) Mtwara imeendesha oparesheni ya kurejesha fedha za korosho zilizofanyiwa ubadhirifu au zilizolipwa kwa baadhi ya watu isivyostahili na kufanikiwa kukusanya shilingi **697,327,187.13.**

Fedha hizi zilikuwa mikononi mwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu ambao wakati wa uhakiki waliongeza majina ya watu ambao hawakuuza korosho katika orodha ya malipo kwa lengo la kujinufaisha baadae, pia wapo waliofanya malipo mara mbili na baadae kuzifuata fedha zilizozidi na kujinufaisha.

Kiasi kingine cha fedha hizo kilitokana na fedha zilizofanyiwa ubadhirifu kwenye baadhi ya vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) katika msimu wa korosho 2017/2018 na 2019/2020. Fedha hizi walipunjwa wakulima kwa visingizio mbalimbali ikiwemo korosho kuibwa zikiwa ghalani na kukosea katika ulipaji mambo yaliyobainika kuwa si ya kweli. Vilevile, zipo fedha ambazo wanachama wa Kiromba AMCOS wilaya ya Mtwara, walikubaliana zikatwe kwa kila kilo ya korosho msimu 2017/2018 ili kuchangia maendeleo ya kijiji, viongozi wa chama hicho katika msimu husika walikata na kuwasilisha fedha pungufu kwa serikali ya kijiji na kufanya ujenzi wa ofisi ya kijiji kutokamilika tangu mwaka 2018. Fedha ambazo hazikuwasilishwa zote zimerejeshwa.

Aidha, fedha zingine zilizookolewa ni shilingi **54,500,000** kutokana na vitambulisho vya wajasiriamali wadogo ambavyo watendaji waliviuza bila kuwasilisha fedha benki. Shilingi **18,518,000** zilikuwa ni kutoka SACCOS ya watumishi wa manispaa ya Mtwara-Mikindani walizokopeshwa watu ambao si wanachama kinyume na taratibu na shilingi **400,000** zilikuwa ni za ushuru wa mbao zilizofanyiwa ubadhirifu kutoka kwa baadhi ya wajumbe wa serikali ya kijiji cha Chinyanyila, wilayani Nanyumbu ambao hawakuziwasilisha serikalini. Hivyo jumla ya Fedha zote zilizookolewa katika kipindi tajwa ni shilingi **770,745,187.13**.

Zoezi la ufuatiliaji wa fedha hizi za korosho ni endelevu kwa kadiri tupatavyo malalamiko pamoja na ukusanyaji wetu wa taarifa za kiintelijensia juu ya mwenendo mzima wa biashara hii katika misimu iliyopita. Tunatoa wito kwa wahusika wote katika tasnia na biashara ya korosho kufanya kazi kwa uadilifu kwani fedha isiyo halali ni moto, itawachoma.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Mtwara iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na rushwa kama yalivyotamkwa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Katika kipindi hicho jumla ya kesi **13** ziliendelea katika mahakama za wilaya za Mtwara, Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba. Vilevile, kesi mpya **3** zilifunguliwa. Kesi hizo ni:

- **Kesi Na.01/2020** iliyofunguliwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mtwara dhidi ya mtumishi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini – LATRA, LUCAS SALUM NUSUHELA, aliyeshitakiwa kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya Rushwa kwa kuomba na kupokea Rushwa ya fedha kiasi cha shilingi 200,000/= toka kwa mtumishi wa basi la abiria la kampuni ya MANING NICE, kinyume na kifungu cha 15(1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

- Ya pili ni **kesi Na.2/2020** iliyofunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Mtwara, dhidi ya MARTIN ABDIEL MUGA - Karani Baraza la Ardhi kwa makosa ya kushawishi rushwa ya shilingi **3,600,000/=** na kupokea Rushwa ya shilingi **300,000**/= kwa kushirikiana na HASSAN AUSI MCHOPA kutoka kwa mteja wa ofisi yake kinyume na kifungu 15(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

- Ya tatu ni **kesi Na. ECC 04/2020** iliyofunguliwa katika Mahakama ya Wilaya Masasi dhidi ya SHAMILA ROSHAN MAJALI na wenzake nane kwa makosa mbalimbali ikiwemo kosa la Kutumia Nyaraka zenye Maelezo ya Uongo Kumdanganya Mwajiri kinyume na vifungu namba 32 na 22 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007, kughushi nyaraka kinyume na vifungu vya 333, 335(a) na 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002, kosa la Utakatishaji wa Fedha Haramu kinyume na vifungu namba 12(e) na 13(a) vya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu Na. 12 ya mwaka 2006 vikisomwa pamoja na Aya ya 22 ya Jedwali la Kwanza na vifungu vya 57(1) na 60(2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kama ilivyorejewa mwaka 2002, kosa la Kusaidia Kutendeka kwa Kosa Kinyume na Kifungu cha 30 cha Sheria Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 ikisomwa pamoja na Aya ya 21 ya Jedwali la Kwanza na vifungu vya 57(1) na 60(2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kama ilivyorejewa mwaka 2002 pamoja na kosa la jumla la kuisababishia hasara serikali kiasi cha shilingi **16,704,316/=** kinyume na Aya ya 10 ya jedwali la kwanza vifungu vya 57(1) na 60(2) vya Sheria ya Uhujumu uchumi sura ya 200 kama ilivyorejewa mwaka 2002.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020 jumla ya taarifa (108) za makosa ya rushwa na makosa mengine ya jinai zilipokelewa na TAKUKURU (M) Mtwara na uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na nyingine watuhumiwa wamefikishwa mahakamani. Mchanganuo wa Sekta au taasisi zinazolalamikiwa ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri, malalamiko (60) katika idara zake kwa mchanganuo ufuatao:- utawala(21), ardhi (12), afya (7), elimu (5), maji(5), kilimo(4), ujenzi(3), biashara(2) na utumishi(1).

Malalamiko mengine ni vyama vya Ushirika malalamiko (34), Polisi(2), Mahakama(1), Siasa (1), LATRA (1), Bima(NIC)(1), Vitambulisho vya wajasiriamali wadogo (1), TRA (1), TAA(1), na binafsi (5).

Ninatoa wito kwa watumishi wa Halmashauri zote za mkoa wa Mtwara na viongozi katika vyama vya ushirika kufanya kazi kwa uadilifu na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kwani takwimu za taarifa za malalamiko dhidi yao ni kubwa.

Ndugu Waandishi wa Habari

Aidha katika kipindi tajwa, ili kuzuia Rushwa, tumefuatilia matumizi ya fedha za Umma katika Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa hapa mkoani Mtwara. Lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa na thamani ya fedha inapatikana. Jumla ya miradi ya maendeleo minane (7) yenye thamani ya jumla ya shilingi **8,886,873,255** ilifuatiliwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

NA	***MRADI***	***THAMANI (Tsh)***
1	*Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa S/sekondari Mangamba -Mtwara*	*55,000,000/=*
2	*Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa S/sekondari Sabasaba -Mtwara*	*54,807,360/=*
3	*Ukarabati wa hosipitali -Nanyumbu*	*400,000,000/=*
4	*Ujenzi wa stendi ya mabasi Mangaka-Nanyumbu*	*2,100,000,000/=*
5	*Mradi wa maji Mwena –Liloya wilaya ya Masasi*	*5,329,673,393/=*
6	*Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi S/sekondari Makukwe-Newala.*	*20,000,000/=*
7	*Mradi wa usambazaji maji kijiji cha Chitandi.*	*927,392,502/=*

Katika miradi tajwa iliyofuatiliwa, mradi wa ukarabati wa hosipitali ya wilaya ya Nanyumbu umeonekana kuwa na tatizo la ucheleweshwaji ambapo pamoja na mzabuni kulipwa lakini baadhi ya vifaa bado havikufika eneo la ujenzi hivyo uchunguzi umeanzishwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kuhakikisha kuwa TAKUKURU inashirikisha umma katika mapambano dhidi ya Rushwa, shughuli za kuelimisha Umma katika kipindi

tajwa zilifanyika kwa kuendesha Semina 44, mikutano ya hadhara 15, Kufungua na kuimarisha Klabu za wapinga rushwa katika shule za Sekondari na Shule za msingi 52, Uandishi wa makala 04, Kuelimisha kupitia vipindi vya redio 03, kufanya Maonesho 04 wakati wa wiki ya sharia na kutoa taarifa 4 kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Aidha jumla ya machapisho 675 yenye elimu dhidi ya rushwa yaligawiwa kwa wananchi

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha kuanzia , Aprili hadi Juni 2020, mikakati ya TAKUKURU Mtwara katika kuzuia na kupambana na rushwa ni pamoja na yafuatayo;

- Kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuwafanya wananchi kuchukua hatua na kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa na kuacha kuwa walalamikaji tu.
- Kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika tasnia ya korosho kwa kuhakikisha kila mkulima anapata stahiki yake.
- Kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi katika sekta za kimkakati za maji, afya, elimu na ujenzi (barabara).
- Kuendelea kufanya chambuzi za mifumo ili kubaini sababu zinazosababisha kuwepo kwa Rushwa na kutoa ushauri wa namna ya kurekebisha au kuboresha na hatimaye kutoa huduma bora.

SHUKRANI:

TAKUKURU (M) wa Mtwara inapenda kuwashukuru wananchi na wadau wote kwa ushirikiano wanaotupatia katika shughhuli zetu na tunaomba tuendelee na moyo huu wa kizalendo.

Pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Ndugu waandishi wa habari kwa ushirikiano wenu na pia nizidi kuwaomba kutuunga mkono katika kutekeleza majukumu yetu kwa kutupatia fursa katika vyombo vyenu ili kuwaelimisha wananchi kuhusu athari na madhara ya rushwa na namna salama na rahisi ya kukabiliana nayo.

"**Kataa Rushwa, Jenga Tanzania"**

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

ENOCK P. NGAILO
KAMANDA WA TAKUKURU (M) MTWARA